# KENYA EDUCATORS CONSULTANCY EXAMS
# KISWAHILI SECTION B ACTIVITIES
# TERM 2 2023

**KISWAHILI SECT. B ACTIVITIES ASSESSMENT**

**NAME**________________________**DATE**__________________

**Jibu maswali YOTE katika nafasi zilizoachwa.**

**SEHEMU YA: A**

**ZOEZI LA I: KUSOMA KWA UFAHAMU**

**1. *Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.***

Chokora ni watoto au familia za mijini. Huwa wachafu kama kilihafu na hawana hela. Utawaona kila mahali katika miji yetu. Huwa hawachagui mahali. Utawaona katika jalala la takataka. Hawachagui ni takataka za aina gani.

Wao huchakura kama kuku takataka na kutafuta vitu. Vitu vinavyotafutwa ni chupa na vinywaji, karatasi za sandarusi au plastiki na vyuma vidogovidogo. Wengine hutafuta vyakula vilivyotupwa.

Watu hawa huzunguka kila mahali wakitafuta riziki. Huonekana kama wendawazimu. Nguo na mwili huwa hakuna tofauti. Uchafu wao huwafanya nzi kuwafuata kila mahali.

Ajabu ni kwamba wao huwa wanafurahia kazi zao. Je, ni kwa nini wako mitaani? Familia zao ziko wapi? Serikali haiwaoni? Maswali ni mengi ambayo kila mtu hujiuliza kuwahusu.

1. Chokora ni nani?____________________________________________ **(Al.1)**
2. Chokora huonekana wapi? ________________________________________ **(Al.1)**
3. Taja kitu kimoja ambacho chokoraa hutafuta wakichokora takataka.______________ **(Al.1)**
4. Kwa nini nzi huwafuata chokoraa kila mahali? ____________________________ **(Al.1)**

**2. *Soma hadithi hii kisha ujibu maswali.***

Nguruwe, ngiri na binadamu walikuwa marafiki wa dhati. Wote walifanya shughuli zao pamoja. Hakika walipendana kama chanda na pete. Nguruwe na ngiri waliishi mwituni kulikokuwa na wanyama wote. Naye binadamu alikuwa na shamba kubwa alilopanda mimea ya aina mbalimbali. Marafiki hawa walitembeleana kila wakati. Ngiri na mwenzake walipomtembelea mja, walipikiwa vyakula vitamu kama halua. Jambo hili liliwafurahisha sana. Naye binadamu alipowatembelea, alionyeshwa mahali kulikokuwa na matunda. Aliyala kwa furaha sana.

Shambani mwa binadamu mlipandwa nafaka na mboga pekee. Nafaka zilipokua, ziliwekwa katika stoo kubwa. Aliwauzia watu sokoni na kupata pesa nyingi. Alijenga jumba kubwa la kuishi.

1. Marafiki hawa walikuwa wangapi?_____________________________ **(Al.1)**
2. Binadamu alipanda nini?___________________________ **(Al.1)**
3. Kisawe cha binadamu ni__________________________________________ **(Al.1)**
4. Binadamu aliweza kujenga jumba kubwa la kuishi kwa sababu

   ___________________________________________________________________ **(Al.1)**

***3.Soma mazungumzo haya kisha ujibu maswali***

**Mwalimu:** Habari za asubuhi?

**Mwanafunzi:** Njema mwalimu. Shikamoo?

**Mwalimu:** Marahaba. Niko salama salimini.

**Mwanafunzi:** Samahani sana. Leo nimechelewa sana.

**Mwalimu:** Kwa nini ukachelewa? (Akitoa mjeledi wake kabatini)

**Mwanafunzi:** (Akilengwalengwa na machozi) Ni-li-a-mka niki-iwa nimechelewa. Jana nililala nikiwa nimechelewa.

**Mwalimu:** Kwa nini ukachelewa kulala? Hujui usingizi ni muhimu?

**Mwanafunzi:** Moto ulikuwa ukiteketeza nyumba ya jirani. Tuliogopa tusipatwe na maafa pia.

**Mwalimu:** Pole sana. Najua alipoteza mali yake. Pia lazima aliumia.

**Mwanafunzi:** Vitu vyote vilichomeka na kuwa jivu. Watu walijaribu kuokoa vitu lakini moto huo ukakataa katakata kuzimika.

1. Je, mwalimu na mwanafunzi walikuwa wapi?___________________________ **(Al.1)**
2. Kwa nini mwanafunzi alichelewa? _________________________________________ **(Al.1)**
3. Ni jambo lipi linaonyesha kuwa mwanafunzi ana adabu?_________________________

   __________________________________________________________________ **(Al.1)**
4. Moto uliteketeza nyumba ya nani?_______________________________ **(Al.1)**

**4. *Soma barua hii kisha ujibu maswali***

Mwanaisha Ali,
S.L.P 56,
Buheri.
12-08-2021.

Kwa rafiki mpendwa Rosa,

Pokea salamu nyingi kutoka kwangu. Mimi ni buheri wa afya. Je, u hali gani mhibu? Natumai kuwa Mungu amekupa afya njema na unaendelea na masomo yako vizuri.

Sababu ya kukuandikia barua hii ni kukuarifu kuwa tumehamia mji wa Buheri. Sababu ya kuuhamia mji huu ni kuwa una shule nzuri na usalama wa kutosha. Mtaa wa Suheli ulikuwa na vioja vingi. Baba na mama waliporwa pesa zote walipokuwa wakielekea nyumbani kutoka kazini.

0724333200 E-mail kenyaeducators@gmail.com. ORDER MARKING SCHEMES
ATwww.kenyaeducators.co.ke or Contact 0724333200/0768321553/0795491185

Jambo hilo liliwakera sana. Walionelea kuuhama kwani wasiwasi umekuwa mwingi. Waja hawalali. Wanaogopa wahalifu hao ambao hawana huruma. Si unamkumbuka Teja ambaye ni mwanabiashara? Walimfumania na kumwacha akiwa hali mahututi. Alipotolewa dukani pake, alipelekwa hospitalini. Pale aliwezwa na akatuaga. Hayupo duniani.

Mambo ni mengi sana lakini muda nao hauniruhusu kukuandikia yote. Kalamu nayo yalilia kichongeo. Ni hayo tu kwa sasa. Tukifunga shule nitaomba ruhusa nikutembelee.

Wako wa dhati,

M.Ali.

1. Barua hii iliandikwa mwezi gani? ________________________ **(Al.1)**
2. Mwandishi walihama kwa sababu gani?________________________ **(Al.1)**
3. Ni nani mwandikiwa wa barua hii? ________________________ **(Al.1)**
4. Teja alikufia wapi? ________________________ **(Al.1)**

**SEHEMU YA B**

**ZOEZI LA II: SARUFI**

**1.** Unda maneno ukitumia sauti hizi

a) dh________________________

b) th________________________

**2.** Kanusha sentensi hii: ***Nikila nitashiba.*** ________________________

**3.** Tunga sentensi ukitumia maneno haya

a) Dania ________________________

b) Kukaanga ________________________

**4.** Pigia mstari nomino za pekee katika orodha hii:

***Jumamosi, Kitabu, Bustani, Juma, Nyumba, Rabuka***

________________________

**5.** Je, maneno haya yako katika ngeli gani?

a) Mwavuli ________________ b) Jua ________________

**6.** Mtu akikuaga **Alamsiki** utamjibu vipi? ________________________

**7.** Tegua kitendawili: ***Popoo mbili zavuka mto.*** ________________________

**8.** Kamilisha nomino ya makundi: ***Tuliona safu ya*** ________________________

**9.** Jaza pengo kwa nafsi inayofaa: ________________ anapenda kucheza soka.

0724333200 E-mail kenyaeducators@gmail.com. ORDER MARKING SCHEMES
AT www.kenyaeducators.co.ke or Contact 0724333200/0768321553/0795491185

**ZOEZI LA iii**

**KUANDIKA** (10mks)

Andika insha ya kusisimua kuhusu

**SHEREHE YA HARUSI**